# Handeni Yetu

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni. Julai- Septemba 2017 Toleo Namba 01

HUTOLEWA KILA BAADA YA MIEZI MITATU



Uchaguzi Mdogo Baraza la Madiwani wafanyika uk 8



Matumizi ya Vitabu vya kukusanyia Mapato sasa Basi Uk 7

Habari Katika Picha Uk 15&16



## Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania amewataka makandarasi wa mabwawa ya Mkata, Manga na Kwandugwa kurudi site kujenga upya UK3



Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. John Pombe Magufuli akizungumza na wananchi wa Kata ya Mkata wakati akiwa Wilayani kulekea Tanga mjini kwenye ufunguzi wa Bomba la mafuta linaloungnisha Tanzania na Uganda.

## YALIYOMO NDANI

Hospitali ya wilaya Mkata ichunguzwe kabla ya kuletewa fedha za Umaliziaji'Ummy Mwalimu". UK4



Wazazi tumieni fursa ya Elimu bure kuhakikisha watoto wanasoma ipasavyo " Martine Shigella" UK5



Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imetakiwa kuhakikisha inatenga 10% ya vijana na Wanawake UK5

Dawa za Minyoo ya Tumbo kwa watoto ni muhimu kwa ustawi wa afya"Mkurugenzi" UK 14



Baraza la Madiwani Limekabidhi Pikipiki kwa Watendaji wa Kata wawili kama Motisha Uk 6





# TAHARIRI

*Karibu mpenzi msomaji wa Jarida la Handeni yetu awamu ya 4 ambapo lengo la jarida letu ni kuwahabarisha wananchi juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kwa kipindi cha miezi mitatu ili iwe nyenzo na daraja la kukuza maendeleo katika Halmashauri . Lengo la Halmashauri ni kuhakikisha kuwa Jarida la Handeni Yetu linapatikana katika kila Ofisi ya Kijiji na Kata ili kuwapa wananchi nafasi ya kusoma na kuelewa namna Halmashauri inavyotekeleza shughuli zake. Aidha tunakaribisha habari na makala mbalimbali kutoka kwenye vijiji na Kata. Makala hizo zinaweza kuelezea jinsi utekelezaji wa miradi na shughuli mbalimbali za maendeleo zinavyofanyika katika Kijiji au Kata husika.*
*Asanteni na tunawatakia usomaji mwema.*




# YALIYOMO

Aliyozungumza Mkimbiza Mwenge Kitaifa mara baada ya Kufungua Bohari yadawa Uk13



Miundombinu ya Barabara Kuboreshwa ili kuinua uchumi waTanzania ya Viwanda uk8



Mkurugenzi atembelea Kata kufuatilia utekelezaji wa maagizo kwa KAMAKAuk10



Wachimbaji wadogo Kwasunga waahidiwa kutoondolewa iwapo watafuata Sheria,Taratibu na KanuniUk10



Mwekezaji Mkomba amepigwa marufuku kufanya shughuli zozote na kufikisha hati miliki ya ardhi ofisini kwa mkuu wa WilayaUK11



Wakulima watakiwa kutumia Mbegu na Pembejeo bora ili kujiinua kiuchumi UK12



LINATOLEWA NA:
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.
S.L.P 355
Handeni, Tanga
Email:ded@handenidc.go.tz
Tovuti: www.handenidc.go.tz
fcebook: handenidc

*DIRA(VISION)*
*Kuwa na jamii iliyoelimika na kuwa na maisha bora.*
*DHAMIRA (MISSION)*
*Kuipatia jamii ya Halmashauri ya Wilaya ya Handeni maisha bora kiuchumi kwa kutumia vizuri rasilimali zilizopo kwa kudumisha Utawala Bora ili kuboresha maisha ya jamii*

# Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania awataka wakandarasi wa mabwawa ya Mkata, Manga na Kwandugwa kurudi eneo la mradi kujenga upya

Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dk.John Pombe Magufuli amewataka wakandarasi wajenzi na washauri waliojenga chini ya kiwango mabwawa ya Manga,Mkata na Kwandungwa kuwepo kwenye site ndani ya wiki 2 ili kujenga mabwawa hayo sawa na kiwango cha fedha ambacho tayari wamelipwa cha Tsh. Bilion 2.8 au kwenda jela kuelezea namna gani watarejesha fedha hizo za watanzania .

Amri hiyo ilitolewa wakati Rais alipokuwa akizungumza na wananchi wa Handeni eneo la viwanja vya Mbwembwele Handeni Mjini akitokea Tanga vilivyoko kwenye uwekaji wa jiwe la Msingi wa Bomba la mafuta Linalounganisha Tanzania na Uganda.

Rais Magufuli alisema kuwa haiwezekani kiasi kukubwa cha fedha kama hicho kulipwa bila kuwepo kwa maji yanayowafikia wananchi.Amewataka wakandarasi hao kuwepo eneo la mradi na kujenga upya mabwawa kwa kutumia fedha zao hadi itakapofikia hatua ya certificate (cheti) ya kulipwa na Serikali Bilioni 1.2 alieleza pia,fedha za watanzania haziendi bure na haiwezekani wananchi wa Handeni kusubiri maji kwa miaka 5 wakati fedha zao tayari zimetumika.

Aidha amewaeleza wananchi kuwa atahakikisha tatizo la maji Handeni linatatuliwa kwasababu kuna miradi mitatu ambayo inatarajiwa kuleta matokeo chanya ikiwemo mradi wa Bilion 2.6 unaomalizikia utakao unganisha maji maeneo ya Manga, Mkata na Handeni, mradi wa zaidi ya Bilion 200 wa maji yatatolewa Pangani na mradi wa Mabwawa hivyo kumaliza tatizo la maji .

Amewataka wakandarasi waliopo na wajao kufanya kazi kwa weledi na kwa wakati ili kufikia malengo yaliyopangwa na kwamba hatakuwa tayari kuwavumilia wakandarasi watakaokwamisha upatikanaji wa maji ya uhakika Handeni.

***"Wakandarasi mliopo na mtakaokuja mkitaka kugombana na mimi chezeni na miradi hii ya maji ya Handeni" alisema*** Rais Dk. John Magufuli.

Kwa upande mwingine amewataka wananchi wa Handeni kuwa wavumilivu na kushirikiana vyema na watumishi wa Afya kwa sababu wanafanya kazi kubwa ya kuwahudumia wagonjwa ikilinganishwa na idadi ndogo ya watumishi iliyopo, amewaeleza kuwa ajira zilisitishwa kwa muda kutokana na zoezi la uhakiki hivyo hivi punde watumishi wa Afya wataongezeka kwani ajira zimekwisha anza kutolewa. Aidha amewataka wananchi kujiunga na mifuko ya bima ya afya ili kuboresha huduma za afya na kuhakikisha wanapata huduma kwa wakati pindi wanapohitaji kuhudumiwa.

Sambamba na hilo Rais amepiga marufuku wafugaji kulisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima na kuwataka viongozi ngazi ya Mkoa na Wilaya kuhakikisha wanasimamia katika kutatua changamoto za wakulima na wafugaji kabla matatizo hayajakuwa makubwa na kugeuka kero,na kuwasisitiza wakulima na wafugaji kuishi kwa amani kwasababu wanategemeana kwa kiasi kikubwa.



Bwawa la Manga

Amewaagiza TAKUKURU kusimamia ili kubaini viongozi wanaopokea rushwa hususani kwa wafugaji ambao wanapesa kwalengo la kupindisha haki za wakulima na wafugaji kiasi cha kupelekea kudumu kwa migogoro ambayo ingeweza kutatuliwa kwa wakati.

Amewataka wananfunzi kuhakikisha wanasoma kwa bidii na kutumia vyema fursa ya elimu bure ili kujiandaa kuwa viongozi wa baadae na kuwaeleza kwamba changamoto ya upungufu ya walimu inakwenda kutatuliwa hivi karibuni kwani ajira zimekwisha tangazwa na zilichelewa kupisha uhakiki wa watumishi waliokuwa wananufaika kinyume cha utaratibu.Amewahakikishia wanafunzi kuwa Serikali imeweka kipaumbele kwenye elimu hususani kwa watoto wa kike.

Mwisho amepongeza wananchi wa Handeni kwa namna wanavyojishughulisha na shughuli za kiuchumi hususani kilimo na ufugaji ambazo ni tija kwa maendeleo yaTaifa letu na kuwataka kuendelea na motisha ya kufanya kazi kwa juhudi huku wakiendelea kulinda amani na umoja uliopo ili kuendeleza Taifa. Rais pia ameahidi kumalizia barabara inayounganisha Dumila na Handeni yenye utrefu wa Kilomita 50 kwa kiwango cha lami ili kurahisisha shughuli za kiuchumi na usafirishaji .

Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. John Joseph Pombe Magufuli alizungumza na wananchi wa Handeni alipokuwa akimalizia ziara yake akitokea Tanga Mjini.

# Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Handeni iliyopo Mkata kuchunguzwa Kabla ya kuletewa fedha za umaliziaji



*Jengo la Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Handeni lililopo eneo la Mkata.*

Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania Dk. Joseph Pombe Magufuli ametoa siku 15 kufanyika kwa uchunguzi wa fedha kiasi cha shilingi milioni 500 zilizotolewa kwaajili ya ujenzi wa Hospitali ya Mkata kufuatiwa kuwepo kwa taarifa za ufujaji wa fedha hizo.

Rais alitoa rai hiyo alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kata ya Mkata alipokuwa akipita kuelekea Tanga mjini kwenye ufunguzi wa Bomba la Mafuta.

Rais Magufuli alisema kuwa uchunguzi ufanyike haraka iwezekanavyo ili fedha nyingine Milioni 800 zilizotengwa kwaajili ya kumalizia jengo hilo la Hospitali ziletwe na kufanyiwa kazi iliyokusudiwa.

Alisema kuwa ataendelea kutumbua majipu hususani wale ambao wamezoea kuiba fedha za miradi ya wananchi hususani za wananchi wanyonge na kwamba anataka watanzania waweze kuifurahia nchi yao.

**"Siku 15 jibu liwe limepatikana ili fedha nyingine zije, kama kuna mkandarasi hafai afukuzwe au mtu mwingine yeyote hafai aondolewe ili tuanze ukurasa mpya , Mkuu wa Wilaya simamia hili kwa sababu lipo ndani ya uwezo wako"**alisema Magufuli

.

Aidha Mh.Rais alisema kuwa kuhusu suala la maji Serikali imeanza kushughulikia likiongozwa na wabunge wa majimbo ya Handeni, kiasi cha Bilioni 2 zimetolewa ili kuhakikisha kwamba tatizo la maji linakwisha na atahakikisha Mkata na Handeni wanaondokana na tatizo hilo.

Sambamba na hilo Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania leo aliwarudishia wananchi wa Kata ya Kabuku ekari 50 za ardhi walizokuwa wamewapa JKT Mgambo zaidi ya miaka 10 kwaajili ya ujenzi wa Kiwanda ambacho hakijaendelezwa, Amewataka JKT kujenga kiwanda ndani ya maeneo yao kwani wanayo maeneo makubwa yenye nafasi za kutosha.

Aidha Mh. Raisi aliwataka wakazi wa Handeni na Tanga kwa ujumla kujipanga kunufaika na fursa ya bomba la mafuta ili kuinua familia zao kiuchumi kwa kufanya kazi kwa juhudi, kulima mazao ya chakula ya kutosha ,amewahakikishia kuwa mradi huu utatoa mchango mkubwa wa kimaendeleo kwa wananchi wa Tanga na Tanzania kwa ujumla.

**" Wananchi na watani zangu Tanga inafunguka kiuchumi, nawahakikishia kwamba mradi huu ni mkubwa na utazidi kuinua uchumi wetu zaidi ya km1000 za bomb la mafuta zinajengwa ndani ya Nchi ya Tanzania tu, watu watafanya biashara, wananchi watapata vibarua na kazi za kudumu"** Alisema

Mwisho aliwataka wananchi wa Tanga kudumisha ummoja na mshikamo kwa kuwatumia vizuri viongozi kwenye kuleta maendeleo na kuwataka vijana kuacha kutumika na watu wasiopenda kuona Tanzania inakuwa na amani, wasidanganywe na vitu vya bure kwani huu ni wakati wa kufanya kazi ili kuweza kupata fedha za halali na kwamba hakuna vitu vya bure.

**"Vijana fanyeni kazi hakuna vitu vya bure msidanganywe na vizawadi vidogovidogo fanyeni kazi, asiyefanya kazi na asile"** Alisema Rais

## Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mh. Martine Shigella amewaasaWazazi kutumia fursa ya elimu bure kuhakikisha watoto wanasoma ipasavyo.

Wananchi Wilayani Handeni wametakiwa kuwapeleka watoto wao shuleni na kutumia fursa ya Elimu bure ili kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata elimu ipasavyo.

Rai hiyo ilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mh.Martin Shigella alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kata ya Kabuku Wilayani Handeni kwenye ziara yake ya Kikazi.

Shigella alisema kuwa Serikali ya awamu ya tano imedhamiria kutoa elimu bure bila malipo kuanzia awali hadi darasa la 12 ni wajibu wa wazazi kuhakikisha watoto wanasoma na Serikali inaweka mazingira mazuri kuhakikisha watoto wanasoma.

Mbali na chanagomoto ya walimu wa kutosha na miundombinu isiyotosheleza na rafiki njia pekee ya kujikwamua na hali hii ni kuhakikisha viongozi wanaelimisha na kuhamasisha wananchi kuchangia nguvu kazi ili waweze kujenga madarasa ya kutosha na hivyo kuondokana na upungufu wa madarasa na vyoo ulipo kwenye shule zetu.

Aliongeza kuwa nchi yeyote duniani haiwezi kuwa na maendeleo kama wananchi wake hawajasoma, lakini tukiwekeza kwenye elimu viwanda vinavyotarajiwa kujengwa vitapata wafanyakazi wanaotokana na elimu tuliyowekeza nchini kwetu.

*"wazazi hakikisheni mnasomesha watoto, mkisomesha watoto mtakuwa na uhakika wa kupata wafanyakazi watakaofanya katika viwanda vinavoanzishwa katika Taifaletu*" Alisema Shigella.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Kiva wakisherehesha kilele juma la Elimu

## Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imetakiwa kuhakikisha inatenga asilimia 10 ya vikundi vya Wanawake na Vijana ili kuinua uchumi wa Tanzania ya Viwanda kwa Wakati.

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imeelekezwa na Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mh. Martin Shigella kutenga asilimia 5 za Vikundi vya kinamama na asilimia 5 kwaajili ya vijana kutoka kwenye mapato yao ya ndani kutokana na bajeti ya Serikali kuu kutotosheleza.

Aliyazungumza hayo alipokuwa akizungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara wa kata ya Kabuku Wilayani Handeni.

Shigella Alisema kuwa lengo la kuitaka Halmashauri kutenga asilimia hizo ni kuunga mkono jitihada za Rais katika kuhakikisha tunakuwa na uchumi wa viwanda kwa kuwa na viwanda vidogovidogo ambavyo vinatokana na nguvu kazi ya vijana na vikundi vya kinamama

Alisema kuwa wananchi wa maeneo ya Mkata wanazalisha kwa wingi na hivyo wanao uwezo wa kuanzisha viwanda vidogovidogo, ndio maana awamu inayokuja fedha zitakazo tengwa badala ya kutoa fedha taslimu kwa vijana na vikundi vya kinamama vitolewe vitendea kazi kama mashine za kufyatulia matofali au mashine za kusagia unga na mashine nyinginezo.

Alieleza kuwa kwa kufanya hivyo wataweza kufikia jitihada za Serikalina hivyo kuhakikisha dhamira ya Rais wetu ya kujenga uchumi wa viwanda inafikiwa kwa wakati.

katika hatua nyingine liwataka vijana na kinamama kuhakikisha wanajisajili kwenye vikundi ili kurahisisha utambuzi wa uwepo wao na iweze kuwa rahisi kwao kupatiwa vibali vya uvunaji wa mazao ya misitu utakaowapa uhalali wa kuvuna mazao hayo ili kuwa na malighafi za uhakika zitakazowasaidia kuendeleza shughuli zao kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni.



Mkuuwa Mkoa wa Tanga Mh. Martine Shigella akiongea na wananchi wa Mkata.

# Baraza la Madiwani limetoa Pikipiki mbili kwa Watendaji wa Kata wawili kama Motisha ya ukusanyaji mzuri wa Mapato.

Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni umetoa pikipiki mbili zenye thamani ya Shilingi Milioni 4 na laki 5 kwa Watendaji wa Kata za Kwasunga na Kang'ata ikiwa ni maagizo ya Baraza la kutoa motisha kwa Watendaji hasa wanaofanya vizuri kazi ya kukusanya mapato na waliopo kwenye mazingira magumu ya kukusanya Mapato .

Motisha hiyo ilitolewa mara baada ya kumalizika kwa Baraza la Madiwani la kufunga mwaka 17/10/2017 lililofanyika kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

Akikabidhi pikipiki hizo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Mh. Ramadhani Diliwa alisema kuwa dhamira yao kama Baraza ni kusaidia na kusimamia shughuli za maendeleo na suala zima la ukusanyaji wa mapato katika kata zote.

Aliongeza kuwa Madiwani wanafahamu kwamba Halmashauri inakipato kidogo , wangengeweza kugawa pikipiki kwa kata zote 21, lakini ni bora kuanza kuliko kuacha kabisa hivyo lazima Madiwani wote waridhie kama walivyopitisha, maana kwa popote zitakapoenda ni Halmashauri ya Handeni na sio mwisho mapato yatakapoongezeka pikipiki zitaendelea kununuliwa ili Kata zote 21 ziweze kupata.

Aidha aliwataka Watendajji kuacha kuchukulia kuwa ni mali ya Serikali na kushindwa kutunza, na kwamba Watendaji wanaokabidhiwa wazitunze ili ziweze kudumu mrefu. **"Watendaji nawaeleza pikipiki hizi zisiwe na mikono mingi, muache kufanyia kazi ambazo hazihusiani na malengo yaliyokusudiwa, kama kupakiza mbao, mikaa,magogo na kadhalika msizichoshe mapema, kafanyieni kazi ya Halmashauri ili zidumu na wengine waje waige kutoka kwenu"** Alisema Mh. Diliwa.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Bw. William Makufwe alisema kuwa wametimiza maagizo waliyopewa na Baraza ya kutoa motisha kwa watendaji watakaofanya vizuri kwenye kukusanya mapato na waliopo katika mazingira magumu hususani pembezoni ambao wanapata changamoto kubwa ya kukusanya mapato.

Aidha alieleza kuwa pikipiki hizo ni mali ya Halmashauri na Kata husika na sio mali ya Mtendaji Kata,lengo ni kusaidia katika shughuli za kukusanya mapato na shughuli nyingine za kiutawala hivyo matumizi binafsi hayaruhusiwi.

Aliongeza kuwa motisha zitaendelea kutolewa kadri fedha zitakapopatikana na Kwamba lengo la Halmashauri ni kuhakikisha Watendaji wote wanapata vitendea kazi ambavyo vitasaidia kuongeza ufanisi wa kazi wakati wowote.

Kwaupande wao watendaji wa Kata za Kwasunga na Kang'ata walipokea kwa furaha vitendea kazi hivyo na kusema kwamba zitawasaidia kufanya kazi kwa bidii na mtawanyiko mkubwa kwenye maeneo yao hali ambayo itapunguza changamoto za ufuatiliaji wa shughuli za mapato na kiutawala katika maeneo yao. Walitoa rai kwa Watendaji wenzao kuongeza juhudi katika kazi kwa bidii na uadilifu ili kufikia malengo ya Halmashauri.
Baraza la kufunga mwaka lilifanyika tare 30-31/8/2017 kwenye ukumbi wa Halmashauri.



Kushoto ni Mh. Diwani wa Kata ya Kwasunga akipokea pikipiki kwa niaba ya Mtendaji wake wa Kata, Kulia ni Mtendaji wa Kata ya Kang'ata Akipokea Pikipiki Kutoka kwa Viongozi Kama Motisha.

# Matumizi ya Vitabu kukusanyia Mapato sasa Basi , Baraza la madiwani limeridhia kwa pamoja.

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Handeni limeridhia kwa pamoja kuacha rasmi matumizi ya vitabu vilivyokuwa vinatumika kukusanyia mapato kwenye baadhi ya Kata, na kutumia mashine za kielekroniki POS(Point Of Sale)kuanzia tarehe 1 septemba 2017.

Makubaliano hayo yalifikiwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani lililofanyika kwenye ukumbi wa Halmashuri, kufuatia Halmashauri kuongeza mashine zingine 50 na kufanya jumla ya mashine 80 ambazo zimesambazwa katika kata zote 21. Mashine hizo zitatumika kukusanyia mapato ambapo kwenye maeneo ambayo yatabainika kuwa na upungufu Halmashauri itaendelea kuongeza mashine.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Mh. Ramadhani Diliwa aliwaeleza Madiwani kwamba, jukumu la kukusanya mapato ni la wote na kila mmoja aone anawajibu wa kushiriki kuhakikisha anasimamia vyema ukusanyaji wa mapato kwa maendeleo ya Halmashauri.

Aliongeza kuwa ukusanyaji wa mapato haujalishi ukubwa au udogo wa Kata, kila Diwani anao wajibu kuhakikisha vyanzo vya mapato vilivyopo katika eneo lake anavisimamia ili hata kidogo kilichopo kiweze kupatikana kwa ukamilifu. Kata zibadilishane mbinu za ukusanyaji wa mapato ili zile zinazoonekana kufanya vyema zisaidie Kata zinazofanya vibaya.



Waheshimiwa Madiwani na Wataalamu Mbalimbali wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni wakiwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani lililoridhia kwa pamoja kutumia mashine za POS kukusanyia mapato la tarehe 31 agosti 2017

Aidha Mwenyekiti alimtaka Mkurugenzi Mtendaji kuhakikisha anafuatilia mienendo ya Watendaji kwa namna wanavyowajibika katika suala la kukusanya mapato ya Halmashauri na kuboresha pale inapobidi. Watendaji watakaoonekana kwenda kinyume na taratibu hatua zakinidhamu zichukuliwe dhidi yao kwa wakati ili iwe fundisho kwa Watendaji wengine.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji Bw. William Makufwe aliwaeleza Madiwani kuwa mashine zimeongezwa ili kuondoa mianya ya ubadhilifu wa mapato ya Halmashuri na kwamba kwa kushirikiana na wataalamu wa mapato watahakikisha mashine zilizotolewa zinatumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Aidha aliwaeleza madiwani kuwa , wataalamu wa mapato na Afisa TEHAMA wataendelea kutoa mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani kila Kata juu ya matumizi ya mashine hizo ili iwe rahisi kwao kuwezakusimamia vyema ukusanyaji wa mapato kwenye maeneo yao.

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ilianza rasmi kutumia Watendaji wa Kata kukusanya mapato ya ndani kuanzia Septemba 1 mwaka 2016 hadi sasa.




Mashine ya POS inayotumika kukusanyia mapato.

## Miundombinu ya Barabara Kuboreshwa ili kurahisisha huduma na kuinua Tanzania ya Viwanda

Mkuu wa mkoa wa Tanga Mh. Martin Shigella amesema kuwa Serikali inampango wa kuboresha miundo mbinu ya Barabara na umeme ili kusaidia kwenye maendeleo ya wananchi katika kuelekea uchumi wa viwanda.

Aliyazungumza hayo alipokuwa kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Kata ya Mkata wenye lengo la kusikiliza kero za wananchi Wilayani Handeni.

Alisema kuwa miundombinu ya barabara ni muhimu katika sekta yoyote ile ya maendeleo ndio maana Serikali inaendelea kujenga barabara bora ambazo zitasaidia wananchi kusafirisha bidhaa zao hususani mazao bila kuharibika.

"Miundombinu ya barabara ikiwa mibovu ,inakuwa ngumu kusafirisha mazao kwa wakati ,na kufikia malengo ya Tanzania ya viwanda" Alisema Shigella.

Aidha alisema Serikali ya Magufuli inadhamira ya kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata umeme katika kila Kijiji ndio maana Serikali imenza ujenzi wa bwawa kubwa la Rufiji ili kuzalisha umeme wa kutosha utakaosambazwa Vijiji vyote na hivyo kuondokana na tatizo la umeme katika maendeleo ya nchi yetu.

Alieleza kuwa tatizo la umeme hususani kwenye Vijijini ni changamoto kubwa mfanoVijiji vya Pozo na Kwasunga vilivyopo Handeni , kwa jitihada za mbunge za kuwapigania wananchi wake, Rea namba 3 itahakikisha umeme unapatikana kwenye Vijiji hivyo na Vijiji 166 vilivyopo Mkoa wa Tanga.

Serikali inatarajia kujenga barabara kwa kiwango cha lami itakayounganisha maeneo ya Mkata ,Kwamasisi na Pangani ili kurahisisha shughuli za maendeleo.



Ujenzi wa Barabara ya Kwamkono -Kweditilibe yenye lengo la kuimarisha usafirishaji na kuboresha huduma za usafiri.

## Baraza la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Handeni limefanya uchaguzi mdogo wa Makamu Mwenyekiti na Wenyeviti wa Kamati mbalimbali.

Baraza la Halmashauri ya Wilaya ya Handeni limefanya uchaguzi mdogo wa Makamu Mweyekiti wa Halmashauri , Wenyeviti wa Kamati zinazoongozwa na Baraza na wajumbe wa kamati husika katika kutekeleza sheria, taratibu na kanuni.

Uchaguzi huo umefanyika mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha Baraza la kufunga mwaka 2016/2017 kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni tarehe 31/8/2017.

Aliyekuwa Makamu mwenyekiti wa Halmashauri ambaye amepata fursa ya kuchaguliwa tena kwa kura 25 kati ya kura 26 Mh. Abdalla Pendeza amewashukuru Madiwani kwa kumwamini na kumpa tena nafasi ya kuongoza kama Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri na kwamba kama walivyoweza kupeleka mbele maendeleo ya Halmashauri vivyo hivyo watarajie mwendelezo wake kwa muhula mwingine wa uongozi.

Aidha amewaomba Madiwani kushirikiana kwa hali na mali ili kuhakikisha wananchi wanaowahudumia wanapata huduma stahiki, kwa wakati na weledi.

Kamati zilizochagua wenyeviti wao ni Kamati ya Huduma za Jamii ( Elimu, Afya na Maji) Mwenyekiti wao ni Mh.David Matula Diwani wa Kata ya Kwankonje,

Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi,Mazingira na Uchumi ni Mh.Joel Mabula, nafasi ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi imebaki kwa Mwenyekiti wa Halmashauri Mh. Ramadhani Diliwa na Kamati ya Ukimwi Mwenyekiti wake amebaki Mh. Abdalla Pendeza.



Makamu Mwenyekiti Mh.Abdalla Pendeza akitoa shukurani

# Wakulima Wilayani Handeni wametakiwa kutumia Mbegu na Pembejeo bora ili kupata mavuno ya kutosha ili kuimarisha uchumi wao

Wakulima Wilayani Handeni wametakiwa kubadili mfumo wa kilimo cha mazoea kwa kutumia mbegu na pembejeo bora ili kupata mavuno mengi na kuondokana na hali waliyonayo ya kuapata mavuno chini ya kiwango .

Hayo yalielezwa na Katibu Tawala Wilaya ya Handeni Bw. John Mahali ambaye pia alikuwa mgeni rasmi kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya kwenye sherehe ya wakulima ijulikanayo kama WAKULIMA FIELD DAY iliyofanyika Kata ya Kabuku iliyoandaliwa na wataalamu wa utafiti wa mbegu ya mahindi ya WEMA kutoka Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika kituo cha utafiti Ilonga.

Katibu Tawala alisema kuwa ni wakati wa wakulima kujipanga kuzalisha zaidi mahindi kwa kutumia mbegu ya WEMA ambayo imeonesha matokeo chanya. Alisema kuwa mbegu ya WEMA itawatoa wakulima kwenye hali ya mavuno machache ambayo walikuwa wanayapata kwa kutumia mbegu za asili.

Aliongeza kuwa wakulima waondokane na kilimo cha kawaida hasa katika kipindi ambacho nchi inaelekea kuwa nchi ya Viwanda, Handeni inapaswa kuwa na viwanda ambavyo vitasaidia kuchakata mahindi ili kuuza unga badala ya mahindi.

Aidha aliwataka wakulima kuangalia namna ambavyo wataweza kutunza chakula ili kuondokana na tatizo la njaa kwa kipindi ambacho mahindi yapo ya kutosha na kuepuka kuyauza yote kwa bei ya chini na kuacha kuweka akiba.

“Kama mkulima umepata mavuno ya kutosha ni lazima kuhakikisha unatenga mazao mengine kwaajili ya chakula kulingana na idadi yako ya kaya, kama unataka kuuza tunza mapka kipindi bei sokoni ipo vizuri” ” Alisema Mahali.

Aidha alitoa rai kwa wazalishaji wa mbegu kupitia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kuweza kufanya mchakato wa namna watakavyoweza kuingia kwenye uzalishaji wa mbegu za WEMA zilizoonesha matokeo chanya kwa lengo la kuwawezesha wakulima kupata mbegu bora za kutosha na kuzalisha mahindi.

Kwaupande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Bw. William Makufwe aliwashukuru wataalamu kutoka Wizarani kwa kuamua kuja kufanya utafafiti kwenye Haalmashauri ya Wilaya ya Handeni kwa Mkoa mzima wa Tanga na kuwaomba watafiti kuhusianisha utafiti na gharama za pembejeo hususani mbegu hiyo ili bei iwe rafiki kwa wakulima wote.



Picha ya zao la mahindi yaliyostawi vizuri.

Alisema kuwa tafiti ndizo zinazopelekea kufanya maamuzi sahihi katika uzalishaji hususani katika zao la mahindi hasa ikizingatiwaa 80% ya wananchi ni wakulima.

Aliomba pia Wizara kuweka utaratibu mzuri wa masoko ya mazao ya wakulima ambayo yamelimwa kama biashara ili kuepuka kuwakandamiza wakulima ambao wametumia nguvu nyingi na gharama kubwa katika kupata mazao hayo.

**“Kwa Handeni mahindi ni zao la biashara ,tuhamasishe uanzishwaji wa viwanda vya kusindika mahindi badala ya mahindi kuchukuliwa hapa na kwenda kuchakatwa kwenye mikoa mingine na kurudishwa tena kama unga”** Alisema Makufwe .

Mkurugenzi wa idara ya utafiti kutoka Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Bw. Jakson Nkuba alisema kuwa lengo kuu ni kuboresha kilimo kupitia uvumbuzi wa mbegu bora zinazovumilia majanga mbalimbali ya magonjwa, ukame na wadudu.

Wizara chini ya idara ya utafiti inalengo la kuhakikisha wakulima wanakuwa na uhakika wa chakula na biashara kwa kujiandaa na viwanda ndio maana wanasisitiza utafiti uendelee.

Aina 11 za mbegu zimefanyiwa utafiti na kutoa matokeo chanya ambapo mbegu ya WEMA inauwezo wa kutoa Tani 4 kwa ekari moja. Utafiti huo unafanyika katika nchi tano yaani Tanzania, Kenya, Uganda, Msumbiji na Afrika ya Kusini.

# Wachimbaji wadogo wa dhahabu waliopo Kwasunga waahidiwa kutokuondolewa

Serikali Wilayani Handeni imewahakikishia wachimbaji wadogowadogo wa madini ya dhahabu zaidi ya 100 waliopo katika Kijiji cha Kwamsampa Kata ya Kwasunga kwamba hawataondolewa kwenye machimbo hayo iwapo watafuata taribu na kanuni walizowekewa.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Handeni Godwin Gondwe alipowatembelea wachimbaji hao na kutoa maagizo ambayo lazima wayafuate kwa usalama wao ikizingatiwa eneo hilo ni la Kijiji na hakuna Mchimbaji Mkubwa yeyote mwenye leseni ya uchimbaji wa madini katika eneo hilo.

Mkuu wa Wilaya aliwaeleza wachimbaji hao kuwa waendelee kuchimba kwa kufuata taratibu za uchimbaji wa madini, wajiweke kwenye kundi kwa kuwa na daftari la majina yao ambalo litafuata taratibu za upatikanaji wa leseni na hatimaye kuwa na leseni halali ya wachimbaji wadogowadogo.

Gondwe aliwataka wachimbaji hao kuacha kukata miti kiholela na badala yake wakate kwa ustaarabu ili waendelee kutunza rasilimali ya miti iliyotunzwa na wanakijiji wa eneo hilo kwa muda mrefu.Aliwaeleza kuwa ni lazima wao kama wachimbaji wa Kata ya Kwasunga watoe ushirikiano na kuheshimu mamlaka ya Kijiji hicho kwa kufuata taratibu watakazopewa.

Kwa upande mwingine Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Bw.William



Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe akizungumza kwamsisistizo na Wachimbaji wa Kijiji cha Kwamsampa,Kwasunga

Makufwe aliwaeleza wachimbaji hao kuwa kile kitakacho zalishwa lazima 20% iende Serikali ya Kijiji na 80% ibaki kwa wachimbaji wenyewe ili kila mmoja apate haki yake kwa utaratibu.

Afisa madini Mkazi Wilayani Handeni Frank Makyao alieleza kuwa ili watambulike kama wachimbaji wa madini ni lazima waunde kikundi ambacho kitasajiliwa na kufika ofisini kwaajili ya kuwekwa kwenye mtandao ambapo itakuwa rahisi kuchukua vipimo na kupata kibali rasmi cha wachimbaji wadogowadogo

Kamanda wa Polisi Wilayani Handeni William Nyelo aliwataka wachimbaji hao kuhakikisha kuwa wanaimarisha usalama wao kwa kutoa taarifa polisi mara tu watakapoona uvunjifu wa amani ikiwa ni pamoja na kutoruhusu wageni kuingia kwenye eneo lao kiholela na kwamba watumie uhuru waliopewa na Serikali kihalali.



Wachimbaji wadogowadogo wa Kijiji cha Kwamsampa kilichopo Kata ya Kwasunga wakichakata madini yao kama inavyoonekana kwenye picha

# Mwekezaji Mkomba apigwa marufuku kufanya shughuli zozote kwenye eneo la uwekezaji

Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe amempa siku 90 mwekezaji anayejulikana kama Hiragro LTD kufikisha hati ya kumiliki ardhi yenye ukubwa wa ekari1000 na kumpiga marufuku kufanya shughuli zozote mpaka atakapokamilisha taratibu za umiliki halali wa ardhi,kabla ardhi hiyo haijarudishwa kwa wanakijiji kwa kushindwa kuendeleza eneo hilo kama walivyokubaliana.

Kauli hiyo aliitoa alipokuwa kwenye kikao baina ya wanakijiji wa Kijiji cha Mkomba kilichopo Kata ya Kwachaga Wilayani Handeni na wawekezaji wa Hiragro LTD ambao waliuziwa eneo hilo mwaka 2013, baada ya wawekezaji kukiuka makubaliano na kuanza kukata miti kwa kuvuna mbao,magogo na kuchoma mikaa kinyume cha makubaliano.

Mkuu wa Wilaya alieleza kuwa ndani ya siku 90 kama hatafikisha hati miliki kwenye ofisi ya Mkurugenzi , ardhi hiyo itafanyiwa utaratibu wa kurudishwa kwa Mkurugenizi Mtendaji ili wapangie mpango bora wa matumizi ya ardhi kwa manufaa ya Kata na Kijiji.

Mh.Gondwe aliwaeleza wanakijiji na viongozi kuwa walifanya makosa kuuza ardhi yenye ukubwa wa ekari 1000 kinyume cha taratibu, hivyo katika kumdai mwekezaji huyo anayedaiwa kuingia kwenye mashamba na makazi ya wanakijiji wanapaswa kufuata taratibu ili kuweza kupata haki zao kwa utaratibu.

Aliongeza kuwa mwekezaji ili afanye kazi ni lazima awe na hati miliki ya eneo na kwamba Serikali na wananchi kwa ujumla wanahitaji



Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe akizungumza na wanakijiji wa Kijiji cha Mkomba, kulia ni Mh.Diwani Kata ya Kwachaga na kushoto Mwishoni ni Muwekezaji kwenye Kijiji cha Mkomba.

mwekezaji lakini, mwekezaji huyo anapaswa kuwa na faida kwa Serikali na jamii inayomzunguka. Mwekezaji akiwa mzuri hata wananchi watanufaika.

Aidha aliwataka wanakijiji kuacha kufanya shughuli kwenye eneo hilo mpaka hapo suluhisho litakapopatikana, na kuwataka kulinda eneo hilo kwa kuhakikisha hakuna shughuli inayoendelea katika eneo hilo na kwamba yeyote atakayekwenda kinyume makubaliano Serikali itachukua hatua.

**"Walinzi wa mali zenu ni ninyi wenyewe, kila mmoja awe mlinzi kuhakikisha kuwa eneo hilo halifanyiwi shughuli tena mpaka suluhu itakapopatikana , mkibaini mtu anakwenda kinyume na utaratibu huu mtoe taarifa na Kamada wa polisi Wilaya atachukua hatua stahiki"** alisema Gondwe.

Kwa upande mwingine Mkurugenzi Mtendaji Bw. William Makufwe alisema kuwa mwekezaji - ahakikishe anapata hati na kuiwasilisha kwenye ofisi yake kinyume na hapo utaratibu wa kisheria utafuatwa ili kumpokonya ardhi hiyo kwa kupeleka pendekezo la kumyangaya ardhi hiyo kwenye baraza la madiwani kwa sababu atakuwa hana hati.

Aidha aliongeza kuwa hata akifanikiwa kuipata hati halali Halmashauri haitaweza kumvumilia kwa kuwa na ekari nyingi,hivyo ekari nyingine zitapunguzwa kwaajili ya maendeleo mengine ya Kijiji.



Mkurugenzi Mtendaji akizungumza na wanakijiji wa Mkomba

# Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni afanya ziara ya kikazi kwenye Kata 10

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmshauri ya Wilaya ya Handeni Bw. William Makufwe amefanya ziara ya kikazi kutembelea Kata 10 yenye lengo la kufuatilia utekelezaji wa maagizo ambayo yalitolewa kutekelezwa na KAMAKA(Kamatai za Maendeleo Kata) ili kutambua wamefikia wapi na muendelezo wao ukoje kulingana na muda uliowekwa kufuikiwa kwa maelekezo hayo.

Wakati wa kufuatilia utekelezaji wa maelekezo hayo Mkurugenzi Mtendaji alizitaka KAMAKA zote kuweka ajenda ya upatikanaji wa chakula shuleni kuwa rasmi kwenye vikao vyao vyote kuanzia ngazi ya Vitongoji hadi Kata na kuhakikisha wazazi wanatambua na kueleweshwa umuhimu wa kuchangia chakula cha watoto wao.

Aliwaeleza KAMAKA kwamba kusomesha watoto ni wajibu wa kila mzazi hususani katika kipindi hiki ambacho Serikali inatoa Elimu bure. Suala la mtoto kupata haki ya msingi ya kufika shuleni na ufuatiliwaji wa maendeleo yake ni la kila mzazi. Watendaji wote ngazi ya Vitongoji hadi Kata wafuatilie kwa karibu na kuwachukulia hatua wazazi wote watakaoonekana wanakwamisha watoto wao kusoma kwa namna moja ama nyingine.

"mzazi/ mwananchi yeyote atakayekuwa kikwazo kwa watoto kusoma na kufikia malengo yao kwa sababu ya mimba Sheria, Taratibu na Kanuni zichukuliwe dhidi yao" Alisema Makufwe.

Aidha aliwataka Maafisa elimu Kata kusimamia majaribio ya mitihani yote yanayotolewa kwenye shule zote ili kuwajengea uwezo wanafunzi na kuinua kiwango cha taaluma. Maafisa elimu wanalazimika kusimamia taaluma kwenye shule zote ili kutoa huduma bora kwa wanafunzi hususani madarasa yenye mitihani ya Taifa ili kujipima ngazi ya Wilaya kabla ya Taifa.

Kuhusu suala la CHF Mkurugenzi Mtendaji alisema wenyeviti na Watendaji wa Kata wanaowajibu kuhakikisha wananchi wanajiunga na mfuko wa afya ya jamii CHF ili kuinua nguvu kazi yenye uhakika wa matibabu . Sula la afya sio la Hiari ni lazima hivyo kila Kata asilimia 50 ya wakazi wote wanapaswa kuwa na kadi za bima ya afya za CHF.

Akielezea suala la ulinzi wa rasilimali za Misitu na maliasili Mkurugenzi aliongeza kuwa kila Kata inawajibu wa kuweka utaratibu wa namna ya kusimamia misitu na maliasili zilizopo kwenye maeneo yao kwa kudhibiti uvunaji wa misitu usiofuata taratibu na kanuni.

Aliongeza kuwa KAMAKA zote zinawajibu wa kusimamia vyema mapato ili Halmashauri iweze kujiendesha yenyewe ikiwa ni pamoja na kuhakikisha fedha zinazoletwa kwenye shule na zahanati zinatumika kwa kufuata sheria taratibu na kanuni ili kuepusha hoja za wakaguzi zinazoweza kuepukika.

Kuhusu suala la kilimo chenye tija Mkurugenzi Mtendaji alisema kuwa wataalamu wa kilimo na mifugo waliopo ngazi ya Kata wahakikishe wanatoa elimu kwa wananchi juu ya kilimo na ufugaji bora utakaoleta tija kwenye maisha na uchumi wa wananchi wote.

Mbali na muitikio mzuri wa Kilimo cha zao la muhogo ekari moja kwa kila kaya Mkurugenzi Mtendaji aliwataka KAMAKA kuhakikisha wanaendelea kusimamia ili zao la muhogo liweze kuwasaidia wananchi kwenye kipindi ambacho mtawanyiko wa mvua hautakuwa wa kutosha na kupelekea upungufu wa chakula.

Usafi wa mazingira ni wajibu wa kila mwananchi na vongozi wanaowajibu kuhakikisha maeneo yanafanyiwa usafi hususani kwenye taasisi za umma na maeneo ya kibiashara . Watendaji wa Kata na Watendajii wa Vijiji wanayomamlaka ya kuwachukulia hatua wale wote watakaokwenda kinyume na kuwataka watekeleze majukumu yao kwa mamlaka waliyopewa.

Aliongeza kuwa Maendeleo ya kila eneo yanaletwa na wananchi wenyewe , Viongozi wote ngazi ya Vitongoji wahamasishe wananchi kushiriki nguvu kazi zao katika kuleta maendeleo kwenye maeneo yao ikiwa ni pamoja na uchangiaji wa matofali kwaajili ya miundombinu ya madarasa na zahanati/vituo vya afya vitakavyojengwa kwenye maeneo yao ambapo kwa sasa ni matofali 25 za kuchoma na matofali 5 za saruji kwa kila kaya.

Mwisho Mkurugenzi alipongeza baadhi ya Kata kwajitihada za kutekeleza majukumu yao na kuzitaka Kata zingine zote ambazo hazijatekeleza, kutekeleza kwa

Inatoka UK12

wakati uliopangwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mkurugenzi Mtendaji alitoa rai kwa Viongozi wote na KAMAKA Kwa ujumla kuwatendea haki wananchi wanaowaongoza na kwamba kila mmoja awajibike kwa nafasi yake kwa kutatua changamoto zinazokabili eneo lake ili kupeleka mbele gurudumu la maendeleo.

Kata 10 za Kabuku nje, Kabuku , Segera, Mazingara, Kwaluguru, Kwamisi, Kwasunga, Komkonga, Mkata na Mgambo zimefikiwa na utaratibu huu utakuwa ukifanyika kila baada ya miezi 3 naMkurugenzi ameahidi kuweka tarehe moja ya kusoma taarifa za mapato na matumizi kwa Kata zote ili kuondoa malalamiko ya wananchi kutosomewa mapato na mtumizi kwa wakati.

## Haya ndiyo aliyozungumza kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa Amour Hamad Amour mara baada ya kuzindua Bohari ndogo ya Dawa




Kiongozi wa mwenge Kitaifa Amour Hamad Amour akizungumza na Kaimu Mkuu wa Wilaya Eng.Gabriel Robert na Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya mara baada ya kufungua Bohari ya Dawa

Kiongozi wa mbio za mwenge wa uhuru kitafa 2017 Ndug. Amour Hamad Amour amepongeza Halmashauri ya Wialaya ya Handeni kwa kufungua Bohari ndogo ya dawa ikiwa ni agizo la Serikali la kuzitaka kila Halmashauri kuwa na stoo za dawa kwenye Hospitali zao.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa bohari hiyo Amour amesema amefurahiswa na mpangilio wa dawa na uwepo wa dawa za kutosha kwenye bohari hiyo na kuwataka wafanyakazi kuhakikisha wanatoa huduma bora kwa wananchi wote bila kujali tofauti zao na kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

Alitoa rai kwa wananchi kutumia dawa hizo kwa kutibu na sio kuzitumia kama chakula cha kawaida, wanapohisi tofauti ya hali zao kiafya wafike hospitali kupata vipimo na maelekezo ya daktari juu ya dawa zipi wanapaswa kuzitumia badala ya kununua dawa wenyewe na kujitibu pasipo kujua tatizo hali inayopelekea kushuka kwa kinga ya mwili kwasababu ya matumizi ya dawa yasiyosahihi.

Amour alitoa wito kwa wataalamu wa afya kuwa dawa zitolewe kwa watu wote hususani pale ambapo kuna utaratibu ambao umepangwa na kwamba kusiwe na kuangalia tofauti zozote za kidini, cheo,,rangi, kabila na kisiasa kwa sababu wananchi wote wanahitaji dawa hizo .

Aliongeza kuwa wananchi waeleweshwe kwamba dawa zote ni sawa , hakuna tofauti kati ya dawa zinazozalishwa hapa nchini na zile za nje ya nchi. Wataalamu wasaidie kuondoa dhana kwamba dawa za nje ni bora na zinanguvu zaidi ya zinazotengenezwa nchini kwetu. wananchi waeleweshwe kuwamba dawa ni dawa bila kujali zimetengenezwa wapi huku akitolea mfano panado ya Kenya inavyoaminiwa na watanzania wengi kuliko panado ya Tanzania.

Amour alieleza kuwa hizi ni zama za kazi na kuwa wagonjwa wanaohudumiwa ndio waliotuajiri hivyo wanapokuja kwenye vituo vyetu kupata huduma, wanatakiwa kuipata katika ubora kwa kuzingatia ubora ambao Serikali imepanga ipatikane kwa wananchi wote. Kila mfanyakazi anao wajibu kufanya kazi kwa bidii bila kujali tofauti na, taratibu zilizowekwa zifuatwe na watu wote isiwe kwa kufahamiana kwani hiyo itakuwa ni moja ya rushwa ambayo Mh. Raisi anaipiga vita.

Inatoka UK 13

Aliongeza kuwa kuboresha huduma kwa wananchi wetu ni suala la msingi kwa sababu tunahitaji kukuza uchumi wa Taifa letu, na ili kufanikisha hilo ni lazima tuwe na afya bora, bila ya afya bora hatuwezi kufanya shughuli yoyote .

"Tujali afya zetu Serikali imedhamiria kuhakikisha huduma zinatolewa kwa usawa kwa watu na wananchi wote ili waweze kupata huduma vizuri ili waweze kuendelea na shughuli nyingine" alisema Amour.

Mwisho aliwataka wananchi na wataalamu kuendelea kutoa vipaumbele kwa wazee na watu wenye mahitaji maalumu wanapokuja kupata huduma kwenye hospitali.

ilielezwa awali kwamba gharama za uanzishwaji wa bohari hii ya dawa ni Tshs 338,254,890/=, ambapo Tshs 9,668,450 ni gharama ya ukarabati wa chumba na uwekaji miundombinu ya kuhifadhia dawa, na Tshs 328,586,440 ni gharama za ununuzi wa dawa na vifaa tiba. Fedha hizi zote ni michango ya wananchi kupitia Mfuko wa Afya wa Jamii CHF, Bima ya Afya ya Taifa na fedha taslimu za malipo ya huduma(papo kwa papo) kwa wateja wasio wanachama wa mifuko ya Bima za Afya.

## Dawa za minyoo ya tumbo ni muhimu kwa watoto kwa ustawi wa Afya zao. " Mkurugenzi Mtendaji"

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni William Makufwe kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Handeni Godwin Gondwe amezindua zoezi la utoaji wa dawa za minyoo ya tumbo katika shule za msingi.

Zoezi la umezaji wa dawa za minyoo ya tumbo umeanza nchi nzima na Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imefungua rasmi zoezi hilo kwenye shule ya Msingi Mkata.

Mkurugenzi Mtendaji alitoa rai kwa wazazi, watumishi wa afya na walimu kuhakikisha wanatoa dawa kulingana na maelekezo waliyopewa kwenye mafunzo waliyopata ya namna ya usimamizi wa zoezi hili. Alieleza kuwa ili kuwa na taaluma nzuri ustawi wa afya ni muhimu kuzingatiwa ikiwamo kumeza dawa za minyoo ya tumbo kwa wanafunzi.

Aliongeza kuwa Serikali inajitahidi kuhakikisha inatoa dawa za kinga ya minyoo ya tumbo na magonjwa ambayo yalikuwa hayapewi kipaumbele kwa ajili ya kuimarisha ustawi wa afya kwa watoto wa shule na jamii nzima ya Tanzania.

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ilianza kutoa dawa za kinga tiba ya ugonjwa wa minyoo katika shule za Msingi mwaka 2016 ambapo kwa sasa jumla ya walimu 234 kutoka katika shule 117 za Msingi zilizopo Wilayani Handeni na watumishi 79 kutoka vituo vya kutolea huduma za afya walipata mafunzo ya jinsi ya usimamizi wa zoezi hili.

Walengwa wa kumeza dawa za minyoo ni wanafunzi wote katika shule zote za Msingi wapatao 72,480 sawa na 100% ya wanafunzi wote wanatarajiwa kupewa dawa na watoto waliofikisha miaka 5 na zaidi ambao bado hawajaingia shule wataruhusiwa kumeza dawa hizi.

Ufunguzi wa zoezi hili ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni na wazazi.



Mkurugenzi Mtendaji Bw.William Makufwe akitoa Dawa kwa mwanafunzi ikiwa ni ishara ya ufunguzi wa zoezi la utoaji chanjo kwa wanafunzi ,shule ya Msingi Mkata.

## HABARI KATIKA PICHA



Viongozi wa Tanga wakiwa kwenye mahojiano na Chombo cha habari TBC wakati wakisubiri ujio wa Rais Mkata.



Mbunge wa Handeni Vijijini Mh. Mboni Mhita akizungumza na wananchi Kwachaga alipopewa nafasi na Rais, kushoto ni Diwani wa Kwachaga



Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mh. Martine Shigella akizungumza na wananchi wa Segera alipofanya ziara ya kikazi Wilayani Handeni.



Raisi wa Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania Dk. John Magufuli akizungumza na wananchi wa Kwachaga akitokea Tanga mjini.



Watendaji wa Kata waliozawadiwa Pikipiki ikiwa ni Motisha kwao, kushoto ni Mtendaji Kata ya Kwasunga na kulia ni Mtendaji wa Kata Kang'ata



Makatibu wa Vikao walioko upande wa kushoto na Afisa Utumishi kulia wakihesabu kura mara baada ya Madiwani kupiga kura zao.

## HABARI KATIKA PICHA



Mkurugenzi Mtendaji Bw.William Makufwe akikagua mradi wa Matofali ya kuchoma ya shule ya Msingi Kwandungwa ikiwa ni utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa alipofanya ziara ya kikazi.



Ukaguzi wa miradi ya maendeleo na Kamati ya FUM(fedha uongozi na mipango)ilipotembelea Bweni la Shule ya Kisaza Sekondari.



Jengo la maabara ya kisayansi Shule ya Sekondari kwaluguru likiwa tayari kufunguliwa na Mwenge wa Uhuru.




Mradi wa Bohari Ndogo ya Dawa uliozindiliwa na mbio za Mwenge wa Uhuru 2017 Halmashauri ya Wialay ya Handeni.



Viongozi mbalimbali na Watumishi wakisikiliza kwa makini ujumbe wa mwenge uliotolewa na Mkimbiza Mwenge Kitaifa Ndg.Amour Hamad eneo la Mkata.



Ufunguzi wa Maaabara ya Sayansi kwa Vitendo Shule ya Sekondari Kwaluguru na Mkimbiza Mwenge Kitaifa wa pili kushoto Amour Hamad Amour.